

ESRF kupitia dira ya maendeleo

Na Hellen Ngoromera

MKURUGENZI wa Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Kijamii na Kiuchumi (ESRF) Dk. Bohela Lunogelo, amesema kuna haja kwa nchi kujipanga upya na kuanzisha kwa umakini masuala mbalimbali mtambuka wakati wa upitiaji upya wa dira ya maendeleo ya taifa ya mwaka 2025.

Dk. Lunogelo alisema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu upitiaji upya wa dira hiyo ya maendeleo ya taifa utakaofanywa kwa uratibu wa ESRF utakaofanywa kwa miezi mitatu.

Alisema pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji wa malengo ya dira yaliyoanza mwaka 2000 ambayo yamefikisha miaka 10 sasa likiwemo ongezeko la uandikishwaji wa watoto katika shule za msingi bado kuna changamoto nyingi zinazolikabili taifa.

Kuhusu mapitio hayo ya dira ya taifa ya alisema

yatalenga kujipima upya nchi ilipofikia katika kuetekeleza malengo yaliyoainishwa na dira hiyo ili kupata picha halisi ya wapi nchi ilipokwama na juhudi zipi na kwa kiwango gani zinahitajika katika miaka iliyobaki.

Jambo lingine litakaloangaliwa katika mapitio hayo ni kutathmini aina ya mafanikio yaliyotokana na sera, mipango na mikakati iliyowekwa na kutekelezwa katika sekta mbalimbali kama sehemu ya kufikia malengo ya dira.

"Tutajifunza jinsi ya kuboresha mikakati ya baadaye au kukwepa kurudia makosa ya nyuma...tunawaomba wananchi wajitokeze kuchangia maoni yao juu ya Tanzania watakayoitaka ifikapo mwaka 2025 kwa masuala ya ubora wa maisha, utawala bora na wa kufuata sheria na mengine," alisema Dk. Lunogelo.

Alisema maoni hayo ya wananchi yatatumwa kwa barua pepe kwao kupitia ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani namba 0652/0767 152 226 au barua pepe tdv2025@esrf.or.tz.